# HALMASHAURI YA WILAYA KISARAWE

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI CHA TAREHE 25/10/2021**

MAHALI: OFISI YA IDARA YA MIFUGO

**KDC/TB/01/../25/10/2021**

**WALIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. James Chitumbi | Afisa Kilimo (W) | Mwenyekiti |
| 2. | Ndg. Alexander Chang'a | Kaimu Afisa Manunuzi na Ugavi (W) | Katibu |
| 3. | Ndg. Ashraf Bigge | Kaimu Mhandisi Ujenzi (W) | Mjumbe |
| 4. | Ndg. Emmanuel Cassian | Afisa Mifugo (W) | Mjumbe |
| 5. | Dr. Libamba Sobo | Mganga Mkuu (W) | Mjumbe |
| 6. | Ndg. Bahati Kikoti | Mwanasheria | Mwalikwa |

SEKRETARIET

1. Mwajabu massenga - Afisa ununuzi

**AJENDA**

1. Kufungua kikao
2. Kupokea Agenda
3. Taarifa ya kitengo cha ununuzi
   a. Maombi ya ununuzi wa kazi ya madarasa 37 ya shule za sekondari Tzs 740,000,000 fedha za uviko kwa mwaka 2021/2022 idara ya elimu sekondari
   b. Maombi ya ununuzi wa kazi za ujenzi wa madarasa matano katika shule ya msingi shikizi ya mzenga 'B' Tzs 100,000,000.00fedha za uviko 19 kwa mwaka 20-21/2022.
   c. Ujenzi wa Nyumba ya Mtumishi 3 in 1 katika cha Afya - Chole Tzs 90,000,000.00 na Ujenzi wa jengo la dharula katika Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe Tzs 300,000,000.00
   d. Ukarabati wa zahanati kuwa kituo cha Afya –Zahanati ya Gwata-Tzs 250,000,000.00
   e. Ukarabati wa zahanati ya Palaka Tzs.160, 000,000.00
   f. Ukarabati wa zahanati ya Kwala Tzs.50,000.00
   g. Ujenzi wa kituo cha Afya cha Kiluvya-Tzs 400,000,000.00
4. Maombi ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi ambavyo vilisahaulika kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya wazazi katika hospitali ya wilaya ya kisarawe na jengo la **OPD.** Tzs 38,015,930.00
5. Maombi ya ununuzi wa ujenzi wa kiwanda cha korosho Tzs 2,000,000,000.00 –Idara ya kilimo
6. mengineyo
7. Kufunga kikao

**KDC/TB/01/1/25/10/2021: KUFUNGUA KIKAO**

Katibu aliwajulisha wajumbe juu ya mabadiliko ya wajumbe wa bodi ambapo alimtambulisha mjumbe mpya ndugu isihaka mbega kutoka kitengo cha uchaguzi aliyebadili nafasi ya mjumbe



Scanned with CamScanner

Ndg.Patrick Gwivaa aliyehamia Morogoro ,pia Ndugu James chitumbi aliyebadili nafasi ya kuwa Mwenyekiti wa bodi .Baada ya maelezo hayo alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 15:15 alasili kwa kuwakaribisha wajumbe katika kikao chakujadili jinsi ya utekelezaji wa miradi ya pesa za uviko.

**KDC/TB/01/2/25/10/2021: KUPOKEA AGENDA**

Katibu alisoma ajenda za kikao ambazo zilikuwa tano wajumbe walizipokea na kuridhia.

**KDC/TB/01/3/25/10/2021: TAARIFA YA KITENGO CHA UNUNUZI**

Katibu aliwasilisha taarifa ya kitengo cha ununuzi na wajumbe walianza kuijadili ukurasa mmoja mmoja.

a. Maombi ya ununuzi wa kazi ya madarasa 37 ya shule za sekondari Tzs 740,000,000 fedha za uviko kwa mwaka 2021/2022 idara ya elimu sekondari
b. Maombi ya ununuzi wa kazi za ujenzi wa madarasa matano katika shule shikizi ya mzenga BTzs 100,000,000.00fedha za uviko 19 kwa mwaka 20-21/2022.
c. Ujenzi wa Nyumba ya Mtumishi 3 in 1 katika cha Afya - Chole Tzs 90,000,000.00 na Ujenzi wa jengo la dharula katika Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe Tzs 300,000,000.00
d. Ukarabati wa zahanati kuwa kituo cha Afya –Zahanati ya Gwata-Tzs 250,000,000.00
e. Ukarabati wa zahanati ya Palaka Tzs.160, 000,000.00
f. Ukarabati wa zahanati ya Kwala Tzs.50,000.00
g. Ujenzi wa kituo cha Afya cha Kiluvya-Tzs 400,000,000.00

Katibu alieleza kuwa tumepokea pesa ambazo zimetolewa na Mh. Rais Samia ambazo ni mkopo kutoka IMF fedha za uviko 19 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na pesa hizo zimeshaingia katika account za shule husika ambapo na maelekezo ya Mh .Rais itumike njia ya Single source na inatakiwa kukamilika tarehe 15/12/2021 .Kitengo kilijadili na kupendekeza kuwa ununuzi kwa ajili ya ujenzi huu ufanyike kwa njia ya moja kwa moja.(single source)kwa kuwa muda ni mdogo hautoshi kutumia njia zingine za ununuzi.

**a).**Maombi ya ununuzi wa kazi ya madarasa 37 ya shule za sekondari Tzs 740,000,000 fedha za uviko kwa mwaka 2021/2022 idara ya elimu sekondari

Madarasa yanayojengwa katika halmashauri ya wilaya Kisarawe ni 37 ya shule za sekondari .kama ifuatavyo hapa chini

| S/N | SHULE | IDADI YA MADARASA |
|---|---|---|
| 1 | KIBUTA | 5 |
| 2 | MZENGA | 3 |
| 3 | GWATA | 3 |
| 4 | GONGONI | 2 |
| 5 | SHULE SHIKIZI YA MZENGA B | 5 |
| 6 | MLOGANZILA | 4 |



Scanned with CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| 7 | MASAKI | 3 |
| 8 | JANGUO | 2 |
| 9 | VIKUMBURU | 2 |
| 10 | MSIMBU | 5 |
| 11 | MFURU | 3 |
| 12 | MANEROMANGO | 3 |
| 13 | MAKURUNGE | 3 |
| 14 | CHOLE | 2 |

**b).** Maombi ya ununuzi wa kazi za ujenzi wa madarasa matano katika shule shikizi ya mzenga B tzs 100,000,000.00fedha za uviko 19 kwa mwaka 2021/2022.

Katibu alitoa ufafanuzi juu ya Maombi ya ununuzi wa kazi za ujenzi wa madarasa matano (5) katika shule shikizi ya Mzenga 'B' Tzs 100,000,000.00 fedha za uviko.19 kwa mwaka 2021/2022 na wajumbe walikubaliana kutumia njia ya kumpata fundi/Mzabuni ni 'Single source'

**c).**Ujenzi wa Nyumba ya Mtumishi 3 in 1 katika cha Afya - Chole Tzs 90,000,000.00 na ujenzi wa jengo la dharula katika Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe .Tzs 300,000,000.00

Mwenyekiti aliwajulisha wajumbe kuwa Idara ya Afya imeomba ununuzi kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa jengo la nyumba ya mtumishi 3in 1–katika kituo cha Afya - Chole Tzs 90,000,000.00 , ujenzi wa jengo la jengo la dharula katika Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe Tzs 300,000,000.00 na kupendekeza kuwa njia ya kumpata fundi na Mzabuni itakuwa 'Single Source'

**d).**Ukarabati wa zahanati kuwa kituo cha Afya –Zahanati ya Gwata-Tzs 250,000,000.00

Katibu aliwajulisha wajumbe kuwa Idara ya Afya imeomba ununuzi kwa ajili ya kazi ya ukarabati wa jengo la zahanati ya Kijiji cha Gwata ni Tzs 250,000,000.00 Fedha hizi zinatokana na tozo za simu na kupendekeza kuwa njia ya kumpata fundi na Mzabuni itakuwa 'Single Source'Baada ya taarifa hiyo hapo juu, wajumbe walishauri watumike mafundi wazoefu na wenye uwezo hasa ambao wamekuwa wanafanya kazi za ujenzi katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri kwa ufanisi mkubwa. Pia, wajumbe walikubaliana namna ya kuwapata ni kuwabainisha na kuwaita mafundi kwa ajili ya kupewa nukuu ya bei ili kupata bei zao kabla ya kuingia mikataba. Mafundi na wasambazaji wanaopendekezwa wameorodheshwa kama ifuatavyo:-

Scanned with CamScanner

ORODHA YA MAFUNDI

| S/N | JINA LA FUNDI | ANUANI/MAWASILIANO | ANAPATIKANA |
|---|---|---|---|
| 1 | Waziri Betera | 0656216737 | Kisarawe |
| 2 | Mshamu Abdallah | 0713545773 | Kisarawe |
| 3 | Ally Mwalimu | 0784272177 | Kisarawe |
| 4 | Harmis Haumotile | | Chanzige |
| 5 | Andrew Laswai | 0713022700 | Dar es salaam |
| 6 | Yusuph Kilimo | 0718 954586 | Kisarawe |
| 7 | Cosmos Lukoo | | Msanga |
| 8 | Ramadhani Mwele | | Msanga |
| 9 | Will John Ndebese | 0784634396 | Kisarawe |
| 10 | Justo Ngumo | 0757913723 | Kisarawe |
| 11 | Frank Akiza | 0787223788 | Dar es salaam |
| 12 | Mustapha | | Kisarawe |
| 13 | Seleman Kizua | | Kisarawe |
| 14 | Baraka Kihame | 0754360242 | Dar-es-salaam |
| 15 | Mazon Balthazari | 0785802919 | Kisarawe |
| 16 | Jaliwa Athuman | 0623944912 | Dar-es -salaam |
| 17 | Ijumaa Abdalah | 0655387338 | Kisarawe |
| 18 | Said Mbande | 0658828228 | Dar-es -salaam |
| 19 | Tito Lazaro | 0782949568 | |

ORODHA YA WAZABUNI

| S/N | Jina La kampuni | Anuani/Mawasiliano | Anapatikana |
|---|---|---|---|
| 1 | Nyeresa General Supply S.l.p 560032 Dar-es-salaam | 0784845709 | Dar-es -salaam |
| 2 | A3 Supply And Hardware S.LP 11077 Dar-es-salaaam | 0713022700 | Dar-es -salaam |
| 3 | Lisangeni Enterprises **S.l.p 25950 Dar-es -salaam** | 07829495 | Dar-es -salaam |
| 4 | Maya General Supply | 071751970 | Dar-es -salaam |
| 5 | Mawegu Enterprises S.l.p | 0754360242 | Dar-es -salaam |

Katibu alipendekeza orodha hiyo wapewe walimu wachague na kuleta majina walioChagua ili kuendelea na taratibu nyingine.

**Azimio**_(a),(b),(c) na (d) utoaji wa orodha ya mafundi na wasambazaji kwa walimu miradi ya UVIKO 19' ufanyike haraka ili kazi isikwame.

e).Ukarabati wa zahanati ya Palaka Tzs.160, 000,000.00

Katibu aliwajulisha wajumbe kuwa Idara ya Afya imeomba ununuzi kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa OPD, nyumba ya mtumishi, kichomea taka na shimo la kondo la nyuma katika zahanati ya Kijiji cha Palaka ambapo fedha zimetolewa na Global Fund' Tzs 160,000,000.00. Kufuatia hela hizi na maelelekezo yake njia ya ununuzi itatumika nukuu ya bei shindani kwa utaratibu wa "Force Account"



Scanned with CamScanner

**…TB/01/5/25/10/2021: MAOMBI YA UNUNUZI WA UJENZI WA KIWANDA CHA KOROSHO TZS 2,000,000,000.00 –IDARA YA KILIMO**

… aliwasilisha maombi ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mtaalamu mshauri na mjenzi wa mradi wa kimkakati wa ujenzi wa kiwanda cha kusindika korosho katika eneo la Vilabwa katika kata ya Mzenga katika Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe. Gharama ya mradi huu itarajiwa kugharimu kiasi cha Tzs 2,824,317,730.00 ambapo, kiasi cha Tzs 1,324,317,730.00 ni kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Kiwanda na ununuzi wa mashine za kusindika korosho na fedha kiasi cha Tzs 1,500,000,000.00 kwa ajili ya ununuzi wa korosho ghafi.

Kwasasa, Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe kupitia Idara ya Kilimo na Ushirika imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 31.56 kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha korosho, ambapo, fedha zilizotengwa kwa awamu ya kwanza, kwa ajili ya kazi hii ni Tzs 2,000,000,000.00

Baada ya kitengo cha ununuzi kupitia maombi haya, ilijadili na kupendekeza kuwa ununuzi wa huduma na ujenzi wa kiwanda hiki ufanyike kwa ngazi mbili ambao hatua ya kwanza ni kupata wataalamu kwa kutumia 'EOI' na hatua ya pili itakuwa kuwapata Wataalamu washauri kwa kuwapa RFP ili kumpata mtaalamu atakaye chora michoro na kutoa mtindo'design' wa majengo ya kiwanda ili kuandaa kabrasha la zabuni. Ambapo, njia ya ununuzi itakayotumika ni ushindani wa kitaifa.

**Azimio-**Wajumbe walishauri ni bora kutafuta mtaalam mshauri kwa ajili ya kufanya kazi hiyo kwa kuwa halmashauri haijawai kuwa na mradi wa aina hiyo.na kisha utaratibu wa kumpata mkandarasi ufanyike.

**KDC/TB/01/5/25/10/2021: MENGINEYO.**

Wajumbe waliomba muhtasari wa bodi uliopita uwasilishwe kwenye kikao kijacho,kuleta circulation zote zilizofanya manunuzi kwa kipindi kilichopita ,na wajumbe walishauri kuwa hawatasaini circulation zozote mpaka circulation zilizopita ziletwe kikaoni ,isipokuwa watasaini circulation za mafuta tu.pia wajumbe wanashauri iundwe kamati ya **CMT** kwa ajili ya kutembelea miradi na ufuatiliaji na kila mjumbe apewe majengo yake kwa ajili ya usimamizi.

**Azimio** :-Iundwe kamati ya **CMT** kufuatilia miradi
-Taarifa za circulation zilizopita ziandaliwe na kuwasilishwa kwenye kikao.

**KDC/TB/01/6/25/10/2021: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 17:15 jioni kwa kuwashukuru wajumbe kwa usikivu, utulivu pamoja na kuchangia mawazo yao.

Muhtasari umethibitishwa:

| | | |
|---|---|---|
| ……………………… | 31/12/2021 ……………… | ……………………… |
| **KATIBU** | **TAREHE** | **MWENYEKITI** |



Scanned with CamScanner